**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/472/SHZ/2023/02**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000119**

**KATI YA**

**NASIB TUNTANGE MBOGELA ............................................... MLALAMIKAJI**

**NA**

**MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA MBEYA (MBEYA WSSA) ..................................... MLALAMIKIWA**

---

**AMRI**

---

***(Imetolewa na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA tarehe 10 mwezi wa Februari 2025)***

**MALALAMIKO HAYA** yameletwa mbele ya Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa ajili ya kutoa uamuzi leo tarehe 10 mwezi wa Februari 2025. Mlalamikaji analalamikia kutozwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya ankara kubwa ya mwezi Februari 2023 kiasi cha TZS 622,261 isiyolingana na matumizi yake ya kila mwezi.

Baada ya kupokea malalamiko, tarehe 13 Machi 2023, Mamlaka (EWURA) ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Taratibu za Kutatua Migogoro Tangazo la Serikali namba 428/2020.

Tarehe 13 Aprili 2023, Mlalamikiwa aliwasilisha utetezi wake na kukiri kupokea malalamiko ya Mlalamikaji.Mlalamikiwa aliendelea kueleza kwamba baaada ya kupokea malalamiko ya Mlalamikaji, alichukua jukumu la kujiridhisha ubora pamoja na utendaji kazi wa dira anayotumia Mlalamikaji. Baada ya uchunguzi, ilithibitika kwamba dira hiyo ina ubora na utendaji kazi wake unaridhisha kabisa na kwamba kiasi chote cha maji kilichosomwa ni sahihi na ankara hiyo ni halali.

Mlalamikiwa ameeleza zaidi kwamba Mlalamikiwa alifika nyumbani kwa Mlalamikaji mara baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa Mlalamikaji na kubaini kuwa kuna mvujo mkubwa wa maji chooni kwa Mlalamikaji kitendo kilichosababisha usomaji kuongezeka na kufikia uniti 5323 kutoka uniti 4846 zilizokuwepo mwanzoni.

Kwamba ni wajibu wa Mlalamikiwa kutoa ankara za maji kwa wateja wake kulingana na kiasi cha usomaji kwenye dira yake, na kutokana na mvujo wa Mlalamikaji kuwa mbele ya dira yake ilisoma matumizi tajwa na kufikia deni analolilalamikia Mlalamikaji.

Vikao vya kutafuta muafaka vilifanyika tarehe 26 Mei 2023 na tarehe 13 Juni 2023 na kuhudhuriwa na pande zote mbili. Katika vikao hivyo, Mlalamikaji aliiambia Mamlaka kwamba Nyumba hiyo wanaishi wapangaji wake ambao ndio watumiaji wa huduma ya Maji inayotolewa na Mlalamikiwa. Tarehe 15 Januari 2025, Mlalamikaji alifika ofisi za EWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na kueleza kwamba ameshamalizana na Mlalamikiwa hivyo hana nia ya kuendelea na shauri, kisha akawasilisha barua ya kufuta shauri.

Katibu wa Bodi **ANATOA AMRI** kwamba malalamiko haya yanaondolewa na kila upande utabeba gharama za uendeshaji wa malalamiko haya.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 10 mwezi wa Februari 2025.

..................................

**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**